# KUKUBALIWA KWA WATU WALIO NA SHIDA YA AKILI WANAPOPATIKANA KATIKA MAENEO YA UMMA

(Sehemu ya 136 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa | |
| 2. Jina la hospitali na wadi | |

## Je! ni kwanini niko hospitalini?

Umeletwa katika hospitali hii na afisa wa polisi kwa sababu tunajali kuwa unaweza kuwa na shida ya akili na unapaswa kuona na mtaalam wa afya ya akili.

Unawekwa hapa chini ya sehemu ya 136 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983 ili uweze kuchunguzwa ili kuona ikiwa unahitaji matibabu.

## Je! nitakuwa hapa kwa muda gani?

Unaweza kuwekwa hapa (au mahali pengine ambapo ni salama) kwa muda wa hadi masaa 72 ili uweze kuangaliwa na daktari na mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa.

Mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa ni mtu ambaye amefunzwa kwa njia maalum kusaidia kuamua ikiwa watu wanahitaji kuwekwa hospitalini.

Ikiwa daktari na mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa wamekubaliana kuwa unahitaji kubaki hospitalini, daktari wa pili anaweza kuulizwa akuangalie ili kudhibitisha uamuzi wao.

Wakati huu haupaswi kutoka isipokuwa uambiwe kuwa unaweza kufanya hivyo. Ukijaribu kutoka, wafanyikazi wanaweza kukuzuia, na ikiwa utatoka, unaweza kurudishwa.

Ikiwa madaktari na mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa hawajakuangalia kufikia mwisho wa masaa 72, utakuwa huru kuenda. Unaweza kuamua kukaa kama mgonjwa wakujitolea. Lakini ikiwa unataka kuenda, tafadhali zungumza na mfanyikazi kwanza.

